

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Baruapepe : [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

*Dar es Salaam*  
*04 Oktoba, 2024*

### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema ili kufikia lengo la kujenga uchumi jumuishi, unaokua kwa kasi, unaoimarisha ustawi wa watu kwa kuboresha huduma za jamii na kupunguza umaskini wa kipato kwa mtu mmojammoja, nchi inapaswa kuwa na mfumo mzuri wa ulipaji na ukusanyaji wa kodi.

Rais Dkt. Samia amesema hayo wakati wa hafla ya uzinduzi wa Tume ya Rais ya Kutathmini na Kushauri kuhusu Masuala ya Kodi iliyofanyika Ikulu.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesema kwa kuzingatia mrejesho na maoni mbalimbali ya wananchi, wadau wa sekta binafsi na wawekezaji wengine, Tume hiyo imeundwa kwa lengo la kufanya tathmini ya mfumo mzima wa kodi, kuimarisha zaidi mfumo huo na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kurahisisha usimamizi wa ukusanyaji wa kodi nchini.

Rais Dkt. Samia amebainisha kuwa licha ya uchumi wa nchi kukua kwa kasi, idadi ya watu kuongezeka na mahitaji ya huduma za jamii na miundombinu kukua, bado asilimia 60 ya uchumi wa nchi unatokana na sekta isiyorasmi.

Rais Dkt. Samia amesema Serikali imedhamiria kujenga mfumo wa kodi unaotenda haki, ambao utamuwezesha kila anayestahili kulipa kodi kulipa kodi stahiki na kutoza kodi zote kwa mujibu wa sheria.

Pia amesisitiza umuhimu wa nchi kuwa na mfumo wa kodi unaochochea ukuaji wa uchumi wa viwanda na kuchangia ujenzi wa uchumi jumuishi, unaoiwezesha Serikali kuwa na vyanzo vya uhakika na vinavyotabirika ili kuleta ustawi kwa wananchi.

Aidha, Rais Dkt Samia ameipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kuiwezesha nchi kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa mwezi Septemba 2024. Amesema hatua hiyo umechangiwa na jitihada za Serikali kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato, kuijengea uwezo TRA, na kuimarisha mazingira ya kufanyia biashara nchini ikiwemo kufuta baadhi ya tozo na kuimarisha utendaji kwenye Idara, Wakala na Taasisi za Serikali.

Jitihada hizo zimeendelea kuleta matokeo chanya ya kuongezeka kwa makusanyo ya kodi na kuongeza ulipaji kodi kwa hiari.

Sharifa B. Nyanga  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

